



Wakati mwengine watu wanasema kuwa “**hawajui jinsi gani ya kuomba**”. Lakini kuomba hakuna ugumu wowote kwani kuomba ni mazungumzo kati yako na Yesu kama rafiki. Wala huhitaji kusema maneno mengi ili Yesu aelewe, bali hata maneno kidogo yanatosha. Yesu anaelewa yote yalioko moyoni mwako. Wala huhitaji sherehe aina yoyote, kwa maana Yesu sio kiziwi. Wewe sema maneno kidogo tu na kuamini Yesu atasikia, kama vile mtoto anapongea na baba yake au mama yake.

**Yesu tafadhali nisaidie kuomba  
na unisaidie kuongea na wewe**